

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018
KUPITISHA MAKADIRIO YA MPANGO NA BAJETI 2017/2018**

A. MATUMIZI YA KAWAIDA NA MISHAHARA (RECURRENT BUDGET)

MISHAHARA	RUZUKU TOKA SERIKALI KUU	JUMLA NDOGO
36,144,906,768	2,608,542,000	38,753,448,768

B. MIRADI YA MAENDELEO (DEVELOPMENT BUDGET)

FEDHA ZA NDANI (Serikali kuu)	FEDHA ZA NJE (Wafadhili)	JUMLA NDOGO
2,318,360,1000	12,621,058,000	14,939,418,000

C. VYANZO MAPATO YA NDANI (OWN SOURCE)

MISHAHARA	O.C	DEVELOPMENT	JUMLA NDOGO
5,304,000	539,637,800	817,412,700	1,362,354,500

D. JUMLA KUU

JUMLA KUU	55,055,221,268
-----------	-----------------------

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KISEKTA KATIKA MWAKA 2015/16 NA JULAI –DESEMBA 2016

Mheshimiwa MwenyeKITI,

Awali ya yote ninapenda kutambua mchango mkubwa wa wadau mbalimbali wa ndani na nje walioshirikiana nasi kwa hali na mali katika kuleta ustawi /mafanikio katika nyanja mbalimbali kupitia michango ya fedha au huduma zao kwa jamii. Kwa kuwataja wachache, Wizara ya fedha , OR-TAMISEMA, OWN-Maafisa, Wizara na Idara mbalimbali za Serikali, Jumuiya ya nchi za Ulaya (EU), Serikali ya Mkoa na Wilaya, World Vision, Shirika la Hifadhi ya Taifa la Wanyamapori- TANAPA, Taasisi za kibenki za NMB na CRDB Kampuni ya Sukari ya ILLOVO, Wananchi wa Kilosa walioshiriki katika sekta za usalishaji na utoaji huduma kwa wananchi; na wafanyabiashara walitoa risiti halali zilizotambulika serikali wakati walipouza huduma au kufanya biashara halali wakiwa na leseni hai.

Kila mmoja wetu ameshiriki kwa namna yake katika upatikanaji wa mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha mwaka moja na nusu (mwaka wa fedha 2015/16 na julai – Desemba 2016/17). Ushiriki wao umewezesha Halmashauri kutekeleza baadhi ya malengo yaliyopitishwa katika mipango yake ya maendeleo na bajeti ya mwaka 2015/16 na 2016/2017.

Muhtasari wa mafanikio wa baadhi ya malengo tuliyoweka ni kama ifuatavyo:-

MALENGO NA MAFANIKIO KISEKTA KUANZIA MWAKA 2015/2016 HADI DESEMBA 2016

NA.	SEKTA	MALENGO	MAFANIKIO
1.	Afya	Kujenga na kukarabati majengo ya kutolea huduma za afya 14 ifikapo Juni 2017	<ul style="list-style-type: none"> Zahanati 3 zimekarabatiwa na Zahanati 6 zimejengwa pamoja na Kituo kimoja cha Afya kimekarabatiwa
2.	Maendeleo ya Jamii	Kutoa msaada kwa WWKMMZ katika Kata 31 kwa kuwalipia ada kwa waliofaulu kwenda kidato cha Tano na kuwapatia vifaa vya Shule ifikapo Juni,2017	Jumla ya watoto 28 wa sekondari waliofaulu kutoka shule za Moro DC na kuijunga na kidato cha Tano, wamechangiwa gharama za ada ambapo Jumla ya Tsh. 3,920,0000 zimetumika
3.	Elimu Msingi	Ujenzi na Uboreshaji wa miundo mbinu katika shule za Msingi	<ul style="list-style-type: none"> Jumla ya madarasa 13 katika Shule za Msingi Bungu, Logo, Nyigwa, Mfungwe, Kiziwa, Singisa na Lumba Juu yamekamilika na yanatumika. Ukarabati wa nyumba za walimu nne zimekamilika katika shule za Msingi Kitengi, Malami zimekamilika na zinatumika.
4.	Elimu Sekondari	Ujenzi na Uboreshaji wa Miundombinu katika shule za Sekondari	<ul style="list-style-type: none"> Ujenzi wa madarasa manne katika shule za Sekondari za Tawa na Kiroka zimekamilika. Ujenzi wa nyumba za walimu (6-1), madarasa (2) na vyoo matundu (10) katika shule ya Tegetero na Bwakila Juu, ujenzi unaendelea. Jumla ya shilingi Milioni 140 kutoka fedha za makusanyo ya ndani zimetolewa kwa ajili yakukamilisha maabara katika Shule za Sekondari 28 na ujenzi unaendelea katika hatua mbalimbali.
5.	Maji	Uboreshaji wa miundombinu ya maji katika vijiji kumi (10)	<p>Jumla ya miradi 10 ipo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:- Mradi wa Kiziwa, Mlilingwa na Chanyumbu imekamilika.</p> <p>Miradi ya Fulwe, Kibwaya, Singisa, Kifindike, Kisaki, Gwata na Mkulazi ujenzi unaendelea.</p>

6.	Ujenzi	Uboreshaji wa miundombinu ya barabara na madaraja	<ol style="list-style-type: none"> 1. Matengenezo ya kawaida km.17 brbr ya UbenaZomozi-Ngerengere imekamilika 2. Matengenezo ya kawaida Barabara ya Mtego wa Simba - Ngerengere km 10 imekamilika. 3. Matengenezo ya muda maalum barabara ya Ngerengere-Kiganila km.9 imekamilika 4. Matengenezo ya sehemu korofi barabara ya Gomero-Nyarutanga km.5 imekamilika 5. Matengenezo ya muda maalum barabara ya Kolero-Kasanga km.4 imekamilika 6. Ujenzi wa nguzo za daraja la Kiroka – Mfumbwe umekamilika. 7. Ujenzi wa daraja la Sesenga – Lumbachini umekamilika.
7.	Fedha/ Biashara	Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani	Halmashauri imenunua mashine za kukusanya mapato kwa mfumo wa kielectroniki (POS 36) zinatumika.
8.	Kilimo	Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagilaji na upatikanaji wa pembejeo za kilimo.	<ul style="list-style-type: none"> • Kazi ya ujenzi wa skimu ya Tulo, Kongwa, na Kiroka unaendelea Jumla ya Kaya 2880 zimenufaika na bolea yakukuzia na Kaya 3333 zimenufaika na Mbegu za Mahindi na Mpunga kwa msimu wa mwaka 2016/17.
9.	Mifugo	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga na kukarabati Majosho. • Kufanya utambuzi na usajili wa Mifugo 	<ul style="list-style-type: none"> • Josho moja limekarabatiwa katika Kijiji cha Kidugalo. • Ng'ombe 6,188 zimepigwa chapa.
10.	Ardhi/Maliasili	Kutoa elimu ya sheria ardhi katika vijiji na kusimamia maliasili, misitu na wanyama pori.	Zoezi la kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa lengo la utatuza wa migogoro ya mipaka imefanyika katika vijiji vya Lubungo, Mfubwe, Mikese, na Newland kwa kushirikiana na Taasisi isiyokuwa ya kiserikali inayoitwa PELUM.
11.	Usafi na Mazingira	Kutoa elimu ya sheria ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira na afya ya jamii	<ul style="list-style-type: none"> • Ukaguzi wa vyanzo vya maji vilifanyika katika tarafa tatu za Mkuyuni, Mvuha na Bwakila • Ukaguzi kwenye maeneo ya machimbo hasa yasiyo

			<p>rasmi umefanyika kwa ajili ya kudhibiti uharibifu uliokithiri kwenye baadhi ya maeneo ya Matombo, Mikesi na Kolero.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Uguzi kwenye viwanda na maeneo ya uwekezaji ya Mkambalani ,Mkulazi na Bwakila umefanyika na kupitia tathimini za athari za kimazingira/Kaguzi za kimazingira
--	--	--	---

CHANGAMOTO

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2015/16 na kipindi cha mwaka cha Julai – Desemba 2016 tumekabiliwa na changamoto nyingi zilizosababisha malengo tuliyojiwekea kutokufikiwa kwa kiwango kilichokusudiwa.

Kati ya changamoto hizo zilikuwa zifuatazo:-

- a) Uhaba wa watumishi katika kada mbalimbali hususan katika sekta ya Elimu, Afya Maendeleo ya Jamii na watakwimu.
- b) Ruzuku iliyodhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi na matumizi mengineyo (OC) kutokutolewa kwa wakati kama ilivyopangwa kwenye mpango kazi.

MIKAKATI ILIYOKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

- a) Kupanga vizuri watumishi maeneo yenyewe upungufu mkubwa. Aidha kuendeleza utaratibu wa kutoa motisha kwa watumishi waliopo na watakaoajiriwa.
- b) Kufuatilia hazina na kwa wadau wengine ili fedha ziweze kutolewa kulingana na mpango kazi kwa kila mwaka.

RASIMU YA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI MWAKA 2017/2018

MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Bajeti ya mapato na matumizi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018 zimetayarishwa kwa kuzingatia mwongozo wa utayarishaji wa mpango na Bajeti wa mwaka wa fedha 2017/2018 na vipaumbele vyta Taifa vilivytotolewa.

VIPAUMBELE VYA KITAIFA

Mpango na Bajeti umezingatia vipaumbele vya kitaifa kama vilivyofafanuliwa katika:-

- a) Mwongozo wa bajeti uliotolewa na OR – TAMISEMI, Tume ya Mipango mwezi Novemba,2016
- b) Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano II 2016/17 – 2020/22
- c) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015
- d) Malengo ya kitaifa ya maendeleo Endelevu (SDGS) -2015- 2030
- e) Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025
- f) Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015.
- g) Masuala ya kijinsia na kinga dhidi ya ukatili wa motto
- h) Masuala ya lishe na kuzuia athari zake.

VIPAUMBELE VYA HALMASHAURI

Halmashauri imezingatia pia Mpango mkakati wake wa mwaka 2016/17 – 2019/22 uliohuishwa mwaka 2016) wakati wa utekelezaji wa vipaumbele vya kitaifa; yafuatayo yamezingatiwa; -

- a) Kuimarisha amani na kuboresha mahusiano baina ya wakulima na wafugaji na wawekezaj hivyo wilaya ya Kilosa kuwa mahala pazuri kwa uwekezaji wowote.
- b) Kuhimiza maendeleo shirikishi katika ngazi zote pasipo kubagua mtu au makundi
- c) Kuboresha ukusanyaji wa kwa kubuni vyanzo vipyta na kutumia mfumo wa kielectroniki wa kukusanya mapato pamoja na kudhibiti matumizi holela
- d) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kubuni vyanzo vy mapato pamoja na utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya wananchi
- e) Kukamilisha miradi mikubwa ya kijamii inayoendelea kutekelezwa hususani katika sekta za afya, maji, elimu na barabara pamoja na kupeleka huduma hizo katika maeneo yaliyokosa huduma, au yenyе hudhuma hafifu.
- f) Kuongeza uzalishaji wa mazao yenyе viini lishe na kuhimiza lishe bora katika kila kaya
- g) Kuendeleza mnyororo wa thamani kwa zao la mpunga, mahindi alizeti na mazao mengine ya kilimo
- h) Kuongeza uzalishaji wa mazao mapya ya korosho, tangawizi na kilimo cha mbogamboga
- i) Kuongeza uzalishaji wa zao la ufuta na mbaazi kwa kusambaza mbegu kwa wakulima
- j) Kushawishi wawekezaji kwa kuboresha miundombinu katika maeneo yenyе fursa za uwekezaji ili waweze kuwekeza kwa ustawi wa wananchi wa Kilosa
- k) Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vya kati na vikubwa vya kuongeza thamani ya mazao na huduma.
- l) Kushughulikia upungufu wa miundombinu hususani majengo, vitendea kazi na samani katika shule za msingi na sekondari
- m) Kushughulikia upungufu wa miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za afya, madawa, vifaa tiba pamoja na kuimarisha Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).
- n) Kupunguza madhara yatokanayo na majanga hususan katika maeneo yanayopatwa na mafuriko kwa kuhimiza Serikali kuu kutenga na kutoa fedha mapema za ukamilishaji ujenzi wa bwawa la Kidete liilopo Wilayani Kilosa na kuimarisha kingo za mto eneo la Kilosa Mjini na Magomeni na mto Mkundi kwa Tarafa ya Magole.

MAOMBI MAALUM

Mh. Mwenyekiti,

Bajeti tunayowasilisha hapa imezingatia ukomo wa bajeti tuliyopewa na Serikali, hata hivyo Halmashauri ina mahitaji ya msingi ambayo hayapo katika bajeti tuliyowasilisha kutohana na ufinyu wa bajeti. Mahitaji hayo tutawasilisha kama maombi maalum Hazina kupitia kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni kama ifuatavyo;

- i. Ujenzi wa jengo la Utawala makao makuu Mvuha5,000,000,000
- ii. Ujenzi wa nyumba za watumishi (wakuu wa idara) Mvuha.....520,000,000
- iii. Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mvuha 700,000,000
- iv. Ununuzi wa Gari la Idara ya Elimu Sekondari..... 170,000,000
- v. Ununuzi wa Gari la Idara ya Elimu Msingi 170,000,000
- vi. Ununuzi wa Gari la Idara ya Utawala(Afyा).....170,000,000
- vii. Ununuzi wa magari mawili (2) ya wagonjwa (Ambulance)340,000,000
- viii. Kulipa madeni ya watumishi wanaohamia Makao MakuuMvuha....900,000,000

Jumla.....Tshs, 7,970,000,000

Mhe, Mwenyekiti,

Makisio ya Bajeti mwaka huu yameongezeka kwa asilimia 27% ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2016/17. Ongezeko hili limetokana na fedha za mfuko wa TASAF awamu ya tatu, ambazo zinakadiliwa kutengwa kiasi cha Tshs.3Bilion kwa ajili ya kusaidia kaya masikini vijijini na bajeti ya Maji ya Tshs. 8 Bilion.

Mhe, Mwenyekiti,

Katika mwaka huu 2017/18 ,Halmashauri imedhamilia kuimarisha huduma za kijamii katika maeneo mbalimbali hasa ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ili kuweza kutoa huduma nzuri kwa wananchi, sekta za Elimu ya msingi, Elimu ya Sekondari hasa kwa kukamilisha ujenzi wa vyumba vyaa maabara,ujenzi wa madarasa, hosteli na nyumba za walimu pia kuongeza kiwango cha ufaulu,kuboresha huduma za afya ,maji na miundo mbinu ya barabara, pia Halmashauri inalenga kutekeleza mikakati yake ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuziimarisha timu za ukusanyaji mapato ya ndani na kuimarisha mfumo wa ulipaji mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

MAPATO KUTOKA VYANZO VYA NDANI VYA HALMASHAURI

Mhe Mwenyekiti,

katika mwaka 2017/2018, Halmashauri inalenga kukusanya mapato ya ndani kiasi cha shilingi 1,960,554,500/- Katika kufanikisha hili mikakati ifuatayo imewekwa kama ifuatavyo;-

- i. Kazi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri itafanywa na Watendaji wa Kata na Vijiji katika maeneo yaochini ya usimamizi wa Waheshimiwa Madiwani.
- ii. Kupitia Sheria ndogo zinazohusiana na viwango vyaa tozo na ushuru, ili kuboresha viwango hivyo.
- iii. Kuongeza nguvu na kuimarisha kikosi cha ukusanyaji Mapato ili kukusanya kwa ufanisi katika vyanzo vya Mapato ambavyo havijabinafsishwa.
- iv. Kuendelea kusimamia Kata ili ziwe na mikakati yake ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ndani ya Kata (kila kata kujua inakusanya kiasi gani cha fedha). Hii ikiwa ni pamoja na Baraza la

- Maendeleo ya Kata kuweka suala la mapato katika agenda za maendeleo ya Kata husika na kubaini mianya yote ya utoroshaji wa mapato.
- v. Kuhamasisha wananchi kuwekeza katika kilimo ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato yatokanayo na kilimo ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wawekezaji wakubwa wanaotaka kuwekeza katika kilimo, mfano Pamba, Ufuta, Vanilla n.k.
 - vi. Kufuatilia na kuchukua hatua za kisheria kwa wafanyabiashara wanaokaidi kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.
 - vii. Kuimarisha masoko kwa kuimarisha miundo mbinu ili kuvutia maeneo ya kufanya biashara na kurahisisha ukusanyaji wa mapato.
 - viii. Kuendelea kufuatilia kwa karibu wadaiwa wote sugu wa Halmashauri ili kulipa madeni yao.

MAOMBI MAALUM

Mh. Mwenyekiti,

Bajeti tunayowasilisha hapa imezingatia ukomo wa bajeti tuliyopewa na Serikali, hata hivyo Halmashauri ina mahitaji ya msingi ambayo hayapo katika bajeti tuliyowasilisha kutokana na ufinyu wa bajeti. Mahitaji hayo tutawasilisha kama maombi maalum Hazina kuititia kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni kama ifuatavyo;:-

i.	Ujenzi wa jengo la makao makuu Halmashauri (w)Mvuha	5,000,000,000
ii.	Ujenzi wa nyumba za watumishi (wakuu wa idara) Mvuha.....	520,000,000
iii.	Ujenzi wa Hospitali	700,000,000
iv.	Ununuzi wa Gari la Elimu Sekondari.....	170,000,000
v.	Ununuzi wa Gari la Elimu Msingi.....	170,000,000
vi.	Ununuzi wa Gari la Afya	170,000,000
vii.	Kulipa madeni ya watumishi.....	500,000,000
Jumla.....		Tsh 7,230,000,000

MWISHO

Mh Mwenyekiti,

pamoja na taarifa hii nimeambatisha mchanganuo wa vyanzo vya mapato ya ndani, shughuli za kawaida za kiidara na mchanganuo wa miradi ya Maendeleo.

Naomba kuwasilisha.

Sudi Mpili
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHURI YA WILAYA YA MOROGORO